HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA 15 CHA MAAFISA HABARI, UHUSIANO NA MAWASILIANO SERIKALINI, UKUMBI WA BOT MWANZA, 18 MACHI, 2019.

Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb.), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;

Mhe. Suleiman Jaffo (Mb.), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI;

Mhe. John Mongela, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza;

Bibi Susan Mlawi, Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;

Ndugu Nicholous B. William, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;

Dkt. Hassan Abbasi, Mkurugenzi, Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali;

Ndugu Paschal Shelutete, Mwenyekiti wa Chama cha Maafisa Habari na Mawasiliano Serikalini (TAGCO);

Watendaji Wakuu Mbalimbali wa Taasisi za Umma na Binafsi;

Maafisa Habari, Uhusiano na Mawasiliano Serikalini;

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana;

Habari za Asubuhi!

SHUKRANI NA PONGEZI

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama jijini Mwanza kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu kwa lengo la kushiriki Kikao Kazi cha 15 cha Maafisa Habari, Uhusiano na Mawasiliano Serikalini.

Pili, namshukuru Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb.), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kunialika ili niweze kushiriki ufunguzi wa kikao hiki muhimu.

Tatu, niwashukuru sana Viongozi wa Mkoa wa Mwanza, kwa kukubali mkutano huu mkubwa kufanyika hapa Mkoani Mwanza.

Nne, naomba mpokee salamu kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Viongozi wetu hao

wanawasalimu na kuwapongeza kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa mbalimbali kwa urahisi na kwa wakati kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo yanayotekelezwa na Serikali.

Ndg. Wanahabri; Kikao hiki kimeandaliwa wakati muhimu kutokana na umuhimu wenu katika tasnia ya habari na umuhimu wenu ndani ya Serikali.

UMUHIMU WA MAAFISA HABARI, UHUSIANO NA MAWASILIANO SERIKALINI

Ndugu Washiriki,

Napenda mfahamu kwamba moja ya sababu iliyonifanya nikubali mwaliko wa kujumuika nanyi kwa kikao Kazi hiki tena bila kusita ni umuhimu wenu kwa Serikali na tutatumia nafasi hii ili kupeana maelekezo kuhusu namna bora ya kutekeleza wajibu wenu wa kisheria na kutekeleza matakwa ya kisheria ya haki ya kupata taarifa. Nimeona mada zilizopangwa ni muhimu na zenye tija sana kwenu.

Kwa lugha nyingine, mwaliko wenu umenipa fursa niliyoitaka ya kutekeleza azma yangu hiyo. Nyote mtakubaliana nami kuwa Maafisa Habari, Maafisa Uhusiano na Mawasiliano Serikalini ni kada muhimu sana katika uendeshaji wa Serikali yetu. Kada hii imebeba wajibu mkubwa wa kuhabarisha umma kuhusu uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi na hivyo, kuisogeza Serikali karibu na umma wa Watanzania.

Ndugu Washiriki,

Kila mmoja wenu anapaswa kufahamu kwamba mkusanyiko wenu huu umekuja wakati muafaka kwani Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi makini wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ipo katika mwaka wake wa nne wa kutekeleza mageuzi makubwa katika kila sekta za kiuchumi na kijamii nchini.

Nyote mnatambua kwamba katika kipindi hiki cha zaidi ya miaka mitatu kazi kubwa tena ya kihistoria imefanywa na

Serikali ya awamu ya tano. Nyie wanahabari ni mashahidi wa haya yanayofanywa. Ni jukumu lenu sasa kuuhabarisha umma wa watanzania kama ambavyo Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyotaka katika Ibara ya 18(d).

Ndugu Washiriki,

Wote mnajua kuwa katika miaka hii mitatu ya mwanzo ya Serikali ya Awamu ya Tano, kumetokea mapinduzi makubwa kwenye kila sekta nchini ikiwemo elimu; afya; nishati; mifugo; viwanda; barabara; viwanja vya ndege; uchukuzi wa anga; uchukuzi wa reli; uchukuzi wa majini; madini; sanaa za filamu na muziki; utalii na michezo mbalimbali.

Hakuna ubishi kwamba ninyi ndiyo wabobezi mnaojua na mnaopaswa kuyatangaza mageuzi haya. Napenda kutumia fursa hii kuwakumbusha kuwa endeleeni kutekeleza vema maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 – 2020

inayoielekeza Serikali kuwatumia ninyi kujenga ushirikiano wa Kizalendo baina ya Vyombo vya Habari vya Umma na vya Binafsi katika kuitangaza Tanzania na mafanikio yake na kujenga taswira ya nchi ndani nan je ya nchi. Kwa kufanya hivyo pia mnatekeleza sharia iliyopitishwa tarehe 1 Septemba, 2016. Sheria ya haki ya kupata taarifa (Access to Information Act of 2016).

Ndg. Wanahabari:

mkumbuke kuwa mnapaswa kuueleza umma wa watanzania kwa kina masuala tunayofanya hususan katika kipindi hiki ambacho Serikali inatekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) wenye kuweka msisitizo kwenye ujenzi wa uchumi wa viwanda. Hakikisheni mnatumia vizuri taaluma yenu na nyezo mnazopatiwa kusema mambo tunayofanya kwenye sekta zote kwani msipofanya hivyo ynayosemwa na wapinga maendeleo yataonekana kuwa ni kweli.

UMUHIMU WA KIKAO KAZI HIKI

Ndugu Washiriki,

Tumieni vema fursa ya uwepo wa kikao kazi pamoja na mambo mengine kujitathmini kwa kina zaidi kuhusu namna mlivyotekeleza wajibu wenu na kutafakari namna bora ya kuyatangaza na kuyatetea mafanikio ya mageuzi makubwa yanayoendelea nchini. Mkumbuke kuwa kazi ya utoaji taarifa kwa wananchi kwa sasa si utashi binafsi wa mtoa habari bali hainabudi kufanywa kwa mujibu wa sheria na Katiba ya Nchi. Mathalan, katika maelezo yangu ya awali, nimeitaja Sheria mpya ya Haki ya Kupata Taarifa Na. 12 ya mwaka 2016 yenye kuzitaka mamlaka za umma kuwapa wananchi taarifa zinazowahusu. Sheria hiyo, inakwenda sambamba na sheria nyingine ya kumlinda mwananchi asilishwe taarifa za uongo, uchochezi na uzushi yaani Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016.

Ndugu Washiriki,

Lengo la Katiba na sheria hizi mbili, pamoja na mambo mengine, ni kuwahakikishia wananchi wetu haki ya kupata habari tena zilizothibitishwa kwa maana ya usahihi wake na kwa wakati. Sababu hizo, ndizo zilizofanya niguswe sana na kauli mbiu yenu isemayo: “UTOAJI HABARI SAHIHI NA KWA WAKATI NI CHACHU KATIKA KUIFIKIA TANZANIA YA KIPATO CHA KATI”. Kaulimbiu hii inakwenda sawa na utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao unalenga kuleta mageuzi ya viwanda nchini.

Katika hili nazipongeza kazi nzuri zinazofanywa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (hususan Idara yake ya Habari - MAELEZO) na timu za habari za viongozi wakuu. Hawa wamekuwa mfano mzuri wa kuigwa wa kutoa habari kwa wakati na usahihi unaohitajika.

Ndugu Washiriki,

Pamoja na kuguswa na kauli mbiu yenu, nimeguswa vilevile na baadhi ya mada ambazo mtazijadili katika kikao kazi hiki. Nimeona mtajadili, pamoja na mambo mengine, dhana ya habari za uongo, kutunga, kughushi na namna kada yenu inavyoweza kusaidia kukidhibiti kichochoro hiki haramu katika habari. Aidha, mtaongezeana ujuzi katika uandishi mzuri wa taarifa kwa umma.

MAELEKEZO MAHSUSI

Ndugu Washiriki,

Kwa kuzingatia matakwa ya Katiba na sheria nilizozitaja hapo awali na kwa kuzingatia kuwa katika baadhi ya ofisi za umma bado kumekuwa na urasimu, natumia fursa ya mkutano huu kutoa maelekezo kama ifuatavyo:

Mosi, viongozi na watendaji wote wa taasisi za umma, kuanzia sasa mshirikiane na maafisa wa habari kwenye maeneo yenu kuhakikisha kuwa habari muhimu kwa

wananchi hazizuiwi kwa urasimu kama hazijazuiwa kisheria. Aidha, habari zitolewe kwa haraka na kwa njia anuai za kisasa.

Pili, Mheshimiwa Waziri wa Habari amekumbusha kuhusu uzinduzi wa tovuti za Halmashauri tulioufanya jijini Dodoma tarehe 27 Machi 2017. Lengo ni kuiongezea Serikali uwezo wa kuwapatia wananchi habari na taarifa kwa haraka kwa kuzingatia kwamba tuko katika kipindi muhimu cha mageuzi katika historia ya nchi yetu ambapo mengi yanafanyika Serikalini ya kiuchumi na kijamii lakini hayafikishwi kwa wananchi! Kuhusu hili, naiagiza Wizara ya Habari kufanya tathmini ya mara kwa mara na kuniletea taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu yenu na matakwa haya ya kisheria miongoni mwa wizara, taasisi za umma na sekretarieti za mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini.

Tatu, Nimemsikia Mhe. Waziri kuhusu changamoto za vifaa mlizonazo na baadhi ya viongozi kutowashirikisha maafisa wao wa habari katika shughuli mbalimbali za Kiserikali ili maafisa hao wawe na taarifa/ habari za kuwapa wananchi. Nitoe maelekezo kwa taasisi zote za

umma nchini kuweka kipaumbele katika kuvinunulia vitengo vya habari vifaa muhimu na kuhakikisha maafisa habari wanashiriki ipasavyo katika hatua zote ili wawe na habari za kuipatia jamii na wanapewa habari kwa wakati. Nanyi wanahabari mnalo jukumu la kuhakikisha vifaa mnavyopatiwa vinatumika kwa masuala yaliyokusudiwa na mnavitunza.

Nne, Viongozi na Maafisa Habari imarisheni mahusiano na mawasiliano Serikalini. Tunahitaji kushirikiana katika kuyatangaza mafanikio lukuki yaliyopo katika taasisi na maeneo yenu. Naagiza kwamba Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano hakikisheni mnatekeleza kazi zenu kwa weledi, uaminifu na uadilifu kwa mujibu wa Sheria, Taratibu, Kanuni na miongozo iliyopo. Vilevile, muwe wabunifu na mhakikishe popote mlipo mnawapatia wananchi haki yao ya kupata taarifa na habari za Serikali kama sheria zinavyotaka.

Tano, Bainisheni vikwazo vya kimuundo, kisera au kisheria, mkutano wenu huu ufanye tathmini ya kina na

kuziainisha changamoto zote na kuziwasilisha Serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kada hii.

Sita, Kila Wizara, Mikoa, Halmashauri na Taasisi zote zihakikishe zinanunua vifaa muhimu vya kufanyia kazi kama vile Kamera, Kompyuta na Simu ili Maafisa habari watekeleze wajibu wao ipasavyo.

MASLAHI YA WATUMISHI

Ndugu Wanahabari:

Serikali inatambua umuhimu wa kama hii katika maendeleo ya nchi. Niwahakikishie kuwa Serikali imeweka Mipango ya kuboresha mazingira ya kazi ikiwemo kutenga fedha za kulipa stahili. Mfano katika kipindi cha Julai-Agosti, 2018, Serikali ilitoa Shilingi Bilioni 184.9 kulipa malimbikizo ya mishahara na madeni mengine yakowemo ya Maafisa Habari na Mawasiliano. Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Motisha na Mishahara inafanya mapitio ya mishahara na motisha mbalimbali kwa watumishi ili kuwa za Usawa na kuendana na kazi.

UMUHIMU WA KUZINGATIA MISINGI YA UADILIFU

Ndugu Washiriki,

UWAJIBIKAJI

Vilevile, ninazo taarifa kuhusu baadhi yenu ambao mnavyo vifaa vyote pamoja na ofisi nzuri zenye kuvutia lakini bado hamtimizi wajibu wenu ipasavyo katika kutangaza shughuli za Serikali. Wengine hawajui shughuli zinazofanywa na Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Wakuu wa Sekta kwa siku, wiki hata mwezi…Taasisi haina taarifa. Badilikeni, nenda mkusanye taarifa na mzitoe hadharani.

Tambueni kwamba Serikali haitowavumilia Maafisa Habari wa namna hii kwani ni wazi kabisa kuwa hawatufai na ni mzigo kwa Serikali. Basi, wale wote wenye mienendo ya namna hiyo chukueni hatua, mjitathmini na mjirekebishe mara moja. Aidha, naielekeza Wizara ya Habari kupitia Idara ya Habari-MAELEZO ifanye tathmini ya kina kuhusu utendaji wa maafisa habari hasa wale wanaoongoza vitengo na watakaoonekana kuwa hawatusaidii tutawaondoa mmoja baada ya mwingine bila kupepesa macho.

Ndugu Washiriki,

Nafahamu pia kuna changamoto nyingine kwa Maafisa Habari ambazo husababishwa na Viongozi au Watendaji

katika Taasisi zetu na hasa katika ngazi za Wizara, Mikoa na Halmashauri. Mara nyingine changamoto hizi huchangiwa na kitendo cha kutotambua mchango wa Sekta ya Habari katika maendeleo ya nchi yetu.

Halikadhalika, ninazo taarifa kuwa wapo viongozi katika wizara, taasisi au mikoa wanafikia hatua ya kutumia waandishi wa habari binafsi badala ya wale waliopo katika utumishi wa umma. Kwanza tabia hii ni hatari kwa usalama wa taarifa za Serikali. Nitumie nafasi hii kukemea viongozi na watendaji wenye tabia za namna hii kuacha mara moja tabia hizo zisizo za kiadilifu. Wizara ya Habari nileteeni majina ya kiongozi au mtendaji wa ngazi yeyote ile ambaye bila sababu zozote hatoi kipaumbele cha kuwatumia wanahabari waliopo katika utumishi wa umma.

Ndugu Washiriki,

Serikali inatumia rasilimali nyingi kuajiri, kuanzisha, kuiendeleza na kuitunza kada ya maafisa habari Serikalini. Hivyo, maafisa habari waliopo washirikishwe vya kutosha ili waweze kushauri na kuhakikisha habari za utekelezaji wa Serikali zinawafikia wananchi badala ya viongozi na wataalamu wengine kukalia habari hizo. Mawaziri na

Wakuu wa Mikoa, Simamieni Maafisa Habari kutimiza wajibuwao.

WANAHABARI NA UZALENDO KWA TAIFA

Ndugu Washiriki,

Kila nchi inayo misingi, utamaduni na tunu zake. Nyinyi ni sehemu ya kundi muhimu sana katika kusimamia na kuendeleza misingi,utamaduni na tunu za Taifa. Hivyo katika kufanya kazi hakikisheni mnabeba agenda za kitaifa. Yapo mambo ambayo ni msukumo wa kitaifa kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Kutokana na haya kila tunachoandika ni lazima kiwiane na agenda zetu kitaifa katika sekta mbalimbali. Kwa mfano: Kisiasa msukumo wetu ni **Amani na utulivu**, Kiuchumi msukumo wetu sasa ni **ujenzi wa viwanda na kulifikisha Taifa katika uchumi wa kati**. Kiutamaduni msukumo wetu ni **Kulinda na Kudumisha** mila na tamaduni zetu. Mambo haya nyinyi mna wajibu wa kuhakikisha mnayapa kipaumbele ili jamii iweze kuhabarishwa vizuri. Vyombo vingine vya nje haviwezi kuyaandika na kuyatangaza mambo haya vizuri na kwa msukumo wa kitaifa kama nyinyi. Nawasihi

chukueni nafasi yenu katika kuzibeba agenda zetu za Kitaifa.

MAENEO MUHIMU YA KUZINGATIA

Ndugu Washiriki,

Nyinyi kama watu mliopata mafunzo ni lazima utendaji wenu ukazingatia maadili na weledi. Wakati wote utekelezaji wa majukumu yenu ujikite katika kuzingatia yafuatayo; Masilahi ya umma, kuepuka uchochezi, kuepuka ushabiki, kuepuka vijembe,na kuepuka kuandika habari zinazopandikiza chuki katika jamii. Aidha, ni muhimu kwenu kuzingatia uaminifu, Haki, Utii, Mahusiano mazuri na Usalama.

MATUMIZI MABAYA YA FEDHA ZA UMMA, RUSHWA NA UFISADI

Ndugu Washiriki,

Mkiwa Maafisa Habari Serikalini mnafahamu vizuri hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma, rushwa na ufisadi. Kwa mfano, Serikali imeokoa shilingi bilioni 19.8 zilizokuwa

zikitumika kulipa wafanyakazi hewa kila mwezi. Vilevile, Serikali imeokoa shilingi bilioni 15.5 kwa kuwaondoa watumishi waliokuwa na vyeti vya kughushi. Kama mtakavyoona, hatua hizo zimeokoa kiwango kikubwa cha fedha ambazo sasa zimeelekezwa katika kujenga na kuboresha huduma nyingine za jamii kwa ajili ya umma wa Watanzania. Sambamba na hayo, Serikali inatekeleza Miradi ya Kimkakati, Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wake kwa Awamu ya Tatu [The National Anti-Corruption Strategy and Action Plan Phase III (NACSAP III 2017/2018 – 2021/2022)]. Tangazeni ili watanzania wajue.

Ndugu Washiriki,

Maeneo mawili yanayowagusa katika utekelezaji wa mpango huo ni mapambano dhidi ya rushwa na kutoa taarifa kwa umma kila mwaka kuhusu namna Wizara na Taasisi zenu zilivyotekeleza mikakati ya kupambana na rushwa. Maafisa Habari wote mnapaswa kuweka mikakati ya kupambana na rushwa katika maeneo yenu ya kazi na kuitekeleza. Huu ni wajibu wenu na iwapo mlikuwa hamuutekelezi kwa kutokujua basi anzeni sasa ili

wananchi wawe mashuhuda wa jitihada hizi zinazochukuliwa na Serikali.

HITIMISHO

Ndugu Washiriki,

Nihitimishe maelezo yangu haya kwa kuipongeza tena Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Msemaji Mkuu wa Serikali, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Chama cha Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini (TAGCO) na wadhamini na watendaji wote wa Serikali mlioshiriki katika maandalizi ya kikao kazi hiki. Nina Imani kitaleta mabadiliko ya kiutendaji Serikalini katika tasnia ya habari.

Kwa msingi huo huo, ni Imani yangu kuwa wote mtatumia muda huu vizuri na kushiriki katika ratiba zilizopangwa kwa ukamilifu bila kutoroka au kuwa na visingizio. Najua Mwanza ni nzuri na kuna vivutio lakini zingatieni ratiba na lengo kuu lililowaleta hapa.

Baada ya kusema haya, nitamke kuwa Kikao Kazi cha 15 cha Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini

kinachofanyika hapa jijini Mwanza sasa kimefunguliwa rasmi.

“Mungu Ibariki Afrika”

“Mungu Ibariki Tanzania”

“Mungu Wabariki Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini”

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA.